

**SHULE YA SEKONDARI THEMI HILL  
MASWALI YA KISWAHILI APR-JUNI, 2020.  
KISWAHILI KIDATO CHA NNE.  
UFAHAMU.**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata.**

Siti alikuwa na tabia ya kujaribiwa ingawa alikuwa mwanamke. Kama wanawake wengine walikuwa na umaskini wa johari hii, yeye alikuwa na ukwasi wake. Alikuwa katika nuru ya tabia wakati baadhi ya wanaume na wanawake walipokuwa katika giza lake. Katika milki kama hii alionekana ana amani na upole, saburi na unyenyekevu, uungwana na uaminifu kwa watu wa kila rika na wa hadhi mbalimbali.

Alikuwa kipenzi kikubwa katika maisha yake, mwanamke huyu alikuwa katika mwendo wa tabia. Kama tabia yake ilihesabiwa kama gari, angalisemwa kwamba gari lenyewe lilitengenezwa vizuri sana. Lilikuwa na kiunzi cha saburi, mtambo wa bidii, magurudumu ya nguvu, sukari ya adili na siwa ya ucheshi. Katika gari hili siti alivuta hewa na maendeleo ya watu toka kila upande kwa kipawa chake kikubwa cha sauti.

Kama Siti hakuwa na tabia ya namna hiyo, tegemeo lake lingalikuwa godo sana katika maisha aliyoshi. Haijulikani angaliwezaje kujiokoa katika hatia isiyosameheka alipokuwa katika hasira na uhungu wa matusi! Hapana sahaka kwa matukano yale yaliyorarua kama kucha za chuma katika moyo wake, alikuwa katika maudhi yasiyoelezeka kwa lugha ya kitabu; lakini alivumilia, alijua kwamba ilimpasa kupigana na wivu, masingizio, kashfa, ujinga wa ulimwengu mzima kama alitaka kufanikiwa. Alikuwa mwanamke mmoja katika wanawake waliokuwa imara kabisa.

Siti alikuwa mwanamke wa tabia kubwa ambayo hakuna kitabu cha Kiswahili kilichofundisha habari zake. Kama aliipata kwa nyumbani au katika unyago inatatiza kuhakikisha kwa sababu wasimulizi wake wote wamenyamaza kimya juu ya jambo hili. Siti hakujua wajibu akaacha kuutumiza. Hakutumia tabia kama kisingizio au joshu baada ya kujichafua kwa tamaa za aibu. Alikuwa na imani nayo siku zote. Hakusema uongo, hakujilegeza, hakujipendekeza wala kujifanya mtumwa. Alifanya kazi kila siku akajipatia ustawi kwa matendo yake mwenyewe. Bila shaka alichukua miaka mingi kufikia ustawi wake, lakini hakushindwa. Na kila siku aliweza kulaza kwa amani kichwa chake juu ya mto bila kusumbuliwa na mawazo mabaya. Lipi lilikuwa bora kwa mwanaume au mwanamke kuliko kutazama nyuma ya maisha yake akayaona safi kama yungiyungi? Siti na tabia yake walikuwa kama marafiki wawili ambao waliafikiana kabisa.

**Maswali:**

1. Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu.
2. Taja sifa kuu tatu (3) za Siti.
3. Nini kiliwavuta watu zaidi kwa Siti?
4. Siti aliwezaje kujistawisha?
5. Mwandishi ana maana gani anaposema “Haijulikani angeweza kujiokoa katika hatia isiyosameheka?”
6. Toa maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

7. Andika ufupisho wa maneno yasiyozidi 45 juu ya aya ya mwisho ya habari uliyosoma.
8. Je, umejifunza nini katika habari ya kwanza uliyosoma?
9. Je, umejifunza nini kutokana na habari ya pili?

#### **SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA**

**Fafanua dhana ya Istilahi zifuatazo kisha toa mfano mmoja kwa kila dhana uliyofafanua.**

10. Mawasiliano
11. Lugha
12. Kamusi
13. Kidahizo
14. Shina
15. Njeo

**Eleza maana ya vidahizo vifuatavyo:**

16. Kinyenyezi
17. Matandu
18. Matlaba
19. Sandali
20. uzimbezimbe
21. Shamirisho
22. Chagizo
23. Prediketa
24. kitomeo
25. Irabu
26. Konsonanti
27. Silabi

**Onesha idadi ya silabi za maneno yaliyopigiwa mstari:**

28. Baba amefuga mbwa mkali
29. Yai la mbuni ni kubwa kuliko la kuku.
30. Haya ni maji ya kunywa tu.
31. Mbuni ukiota unaishi miaka mingi
32. Ugonjwa wa kipindupindu husababishwa na nzi.
33. Nini maana ya mzizi waneno?.....

**Onesha mizizi ya maneno yafuatayo.**

34. Salisha
35. Anakunywa
36. Onyesha
37. Onesha
38. Eleza maana ya utata.

**Istilahi zifuatazo zina utata,toa maana mbili kwa kila Istilahi.**

39. Nyanya
40. Paa
41. Ua
42. Tai
43. Panga

44. Kanga
45. Kaa

**Andika tungo zifuatazo kwa usahihi:-**

46. Mwenyekiti alihairisha mkutano.
47. Mtoto amedumbukia shimoni
48. Kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia deksi moja.
49. Kesho nitanunua dazani ya sufuria.
50. Mvulana mrembo alipita hapa asubui.
51. Kule shimoni mna nyoka.
52. Jana asubuhi apakuwa na chakula chochote kile.

**Tunga sentensi mbili kwa kila kiunganishi kifuatacho:**

53. Ingawa
54. Kwa sababu
55. Lakini
56. Vile
57. Na

Urudufishaji ni njia mojawapo ya uundaji wa msamiati Katika lugha ya kiswahili. Eleza maaana ya urudufishaji kisha rudufisha maneno yafuatayo:-

58. Katika
59. Vile
60. Huko
61. Pole
62. Haraka

**Tungo zifuatazo ni tata, eleza maana ya utata kisha toa maana mbili kwa kila tungo;-**

63. Ali anampenda dada yangu.
64. Nyumba ile ni ya wageni.
65. Juma ana ua nyumbani kwake.
66. Atakuja jumanne.
67. Mwalimu ameacha kazi
68. Kaka ana nyanya.
69. Jana niliona paa.
70. Nimenunua paa.....
71. Usisahau kuchukua pamba
72. Ukija njoo na nyanya
73. Tafadhali usinivunjie nyumba yangu
74. Daktari ataniunga mkono.

**Andika maneno kaa na tupa katika sentensi zifuatazo:**

75. Tafadhali kaa hapa unisubiri.
76. Nolea tupa kisu hicho.
77. Watu wengi hula paa.
78. Kama umeshiba tupa kilichobaki.
79. Ukila kaa chini usisimame.

**Fafanua maana ya neno bichi na moto katika sentensi zifuatazo**

**003** Udongo uwahi ungali **mbichi**

80. Kijana huyu ni **moto**

81. Nipatie maji ya **moto**
82. Ugali huu ni **mbichi**
83. Nipatie maziwa **mabichi**

**Eleza matumizi ya neno “*kwa*” katika sentensi zifuatazo:**

84. Walikusanyika wazee **kwa** watoto
85. Nimekuja **kwa** miguu
86. Unatakiwa uende **kwa** mwalimu.
87. Amekuja **kwa** wito wako.
88. Mgonjwa amekula **kwa** shida.

**Onesha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi zifuatazo:-**

89. Nilimuona Juma nilipofika Mbeya.
90. Ng’ombe aliyepita ameumia mguu.
91. Kule alikokwenda jana kulikuwa na bidhaa nyingi.
92. Kijana ambaye alitusimulia habari zake juzi amepata zawadi ya bahati nasibu ya Taifa.
93. Rejesta ni nini?

**Eleza kwa mifano kuonesha rejesta inayotumika katika sehemu zifuatazo:**

94. Hotelini
95. Mahakamani
96. Sokoni
97. shuleni
98. Hospitalini
99. Ndani ya mabasi